Hati Muhimu kwa Wagonjwa Na Wazazi/Walezi

Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA) Ya Remdesivir Kwa Ugonjwa wa Virusi Vya Korona 2019 (COVID-19)

Umekuwa unapewa dawa inayoitwa **remdesivir** kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa wa virusi vya korona 2019 (COVID-19). Hati hii muhimu ina taarifa za kukusaidia kuelewa hatari na faida za kutumia remdesivir, ambazo umepata au unaweza kuzipata.

Hakuna bidhaa iliyopo iliyothibitishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Chakula na Dawa ya Marekani (FDA) kutibu COVID-19. Kutumia remdesivir kunaweza kuwanufaisha baadhi ya watu wenye COVID-19 hospitalini. Soma Hati hii Muhimu kwa maelezo kuhusu remdesivir. Zungumza na mtoa huduma za afya wako ikiwa una maswali yoyote. Ni chaguo lako kutumia remdesivir au kuacha wakati wowote

Je, COVID-19 ni nini?

COVID-19 inasababishwa na virusi vinavyoitwa virusi vya korona. Aina hii ya virusi vya korona havijawahi kuonekana kabla. Virusi hivi vipya vya korona kwa mara ya kwanza vilikutwa kwa watu huko Wuhan, Jimbo la Hubei, China Desemba 2019. Kuenea kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kuliripotiwa nje ya Hubei na katika nchi nje ya China, ikiwemo Marekani. Unaweza kupata COVID-19 kwa kukaribiana na mtu mwenye virusi.

Ugonjwa wa COVID-19 up kati ya homa kidogo sana (ikiwemo baadhi bila kuwa na dalili iliyoripotiwa) hadi homa kali, ikiwemo homa inayosababisha kifo. Wakati taarifa hadi sasa inasema kwamba wagonjwa wengi wa COVID-19 ni wa homa kidogo, homa kali inaweza kutokea na inaweza kusababisha baadhi ya matatizo yako ya afya kuwa mabaya zaidi. Wazee na watu wenye umri wote homa kali, tatizo la afya la muda mrefu (sugu) kama vile ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa mapafu na kisukari, kwa mfano, wanaonekana wako hatarini zaidi kulazwa kwa sababu ya COVID-19.

Je, zipi ni dalili za COVID-19?

Dalili za COVIDI-19 ni homa, kikohozi na kupumua kwa shida, ambazo zinaweza kutokea siku 2-14 baada ya kupata maambukizi. Homa kali ikiwemo matatizo ya kupumua yanaweza kutokea na yanaweza kusababisha matatizo mengine ya kiafya kuwa mabaya zaidi.

Je, remdesivir nini?

Remdesivir ni dawa ya kupambana na virusi inayofanyiwa uchunguzi ili kutibu baadhi ya watu wenye COVID-19 waliolazwa hospitali. Remdesivir ni dawa inayofanyiwa uchunguzi kwa sababu bado inafanyiwa utafiti. Kuna taarifa chache inayofahamika kuhusu usalama na ufanisi wa kutumia remdesivir kutibu watu wenye COVID-19 waliolazwa hospitali. Remdesivir imeonyesha kwenye majaribio ya tiba kupunguza muda wa kupona kwa baadhi ya watu. Hakuna dawa iliyothibitishwa na FDA kuwa salama na fanisi kutibu watu wenye COVID-19 waliolazwa hospitali. Hata hivyo, FDA imeidhinisha matumizi ya dharura ya remdesivir kwa ajili ya kutibu COVID-19 chini ya Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA). Kwa taarifa zaidi kuhusu EUA, angalia kipengele cha "**Idhini ya Matumizi ya Dharura ni nini (EUA)?**" mwishoni mwa Hati hii Muhimu.

Je, ninapaswa nimwambie nini mtoa huduma za afya wangu kabla sijatumia remdesivir?

Mwambie mtoa huduma za afya wako kuhusu matatizo yako yote ya afya, ikiwemo kama:

- Una mizio yoyote
- Una matatizo ya figo au ini
- Una ujauzito au unapanga kuwa mjamzito

- Unanyonyesha au unapanga kunyonyesha
- Una homa yoyote kali
- Unatumia dawa yoyote (agizo la daktari, kununua dukani, vitamini, au bidhaa za miti shamba)

Nitatumiaje remdesivir?

Remdesivir unapewa kupitia mshipa wa damu (katika mishipa au IV) mara moja kila siku kwa hadi siku 10 kutegemeana na kile anachofikiri mtoa huduma za afya wako kuwa kinafaa zaidi kwako. Remdesivir inaweza kusaidia kupunguza kiwango cha virusi vya korona mwilini mwako. Hii inaweza kukusaidia ahueni haraka.

Je, madhara muhimu yanayoweza kusababishwa na remdesivir?

Madhara muhimu yanayoweza kusababishwa na remdesivir ni:

- Athari inayohusiana na unywaji wa dawa. Athari inayohusiana na unyweshaji dawa imeonekana wakati wa unyweshaji remdesivir au wakati wote ulipopewa remdesivir Ashara na dalili za athari inayohusiana na unyweshaji dawa zinaweza kujumuisha: msukumo mdogo wa damu, kichefuchefu, kucheua, kutoka jasho, na kutetemeka.
- Kuongezeka kwa viwango vya mmeng'enyo wa ini. Kuongezeka kwa viwango vya mmeng'enyo wa ini kumeonekana kwa watu ambao wametumia remdesivir, ambayo inaweza kuwa ishara ya uvimbe-uchungu au kuharibika kwa chembe hai kwenye ini. Mtoa huduma za afya wako atakufanyia vipimo vya damu ili kuangalia ini lako kabla ya kutumia remdesivir na kila siku wakati unatumia remdesivir.

Hizi sio athari zote zinazoweza kusababishwa na remdesivir. Remdesivir bado inafanyiwa utafiti hivyo kuna uwezekano kwamba hatari zote hazijulikani kwa sasa.

Sio watu wengi waliotumia remdesivir. Athari kubwa na zinazotarajiwa zinaweza kutokea. Athari ya kutumia dawa yoyote kwa mshipa wa damu inaweza kujumuisha maumivu ya muda mfupi, kutokwa damu, kuvilia ngozi, uchungu, kuvimba,na uwezekano wa maambukizi kwenye sehemu iliyochomwa sindano.

Je, machaguo mengine ya matibabu ni yapi?

Kama ilivyo remdesivir, FDA inaweza kuruhusu matumizi ya dharura ya dawa nyingine kutibu watu wenye COVID-19 hospitali. Nendwa kwenye www.cdc.gov/COVID19 kwa maelezo kuhusu matumizi ya dharura ya dawa nyingine ambazo hazijaidhinishwa na FDA kutibu watu wenye COVID-19 hospitali. Mtoa huduma za afya wako anaweza kuzungumza na wewe kuhusu majaribio ya tiba ambayo unaweza kustahiki.

Ni chaguo lako kutibiwa au kutotibiwa na remdesivir. Unaweza kuamua kutoitumia au kuacha kuitumia wakati wowote, haitabadilisha viwango vyako vya huduma ya matibabu.

Itakuwaje iwapo nitaamua kutotumia remdesivir?

Ikiwa hautamii remdesivir, unaweza kuumwa zaidi au hata kufa. Hata kama unatumia remdesivir haswa kama ulivyoelekezwa kutibu COVID-19, bado kuna uwezekano wa kuumwa zaidi au kufa.

Je, itakuwaje iwapo mimi ni mama mjamzito au ninanyonyesha?

Kuna uzoefu mdogo wa kutoa remdesivir kwa wanawake wajamzito au mama wanaonyonyesha. Kwa mama na mtoto ambaye hajazaliwa, faida za kutumia remdesivir zinaweza kuwa kubwa kuliko hatari itokanayo na matibabu. Ikiwa wewe ni mjamzito au unanyonyesha, jadili machaguo yako na hali mahususi na mtoa huduma ya afya wako.

Ninatoaje taarifa ya athari ya remdesivir?

Mwambie mtoa huduma za afya wako mara moja iwapo una athari ambazo zinakusumbua au haziishi.

Toa taarifa ya athari kwenda **FDA MedWatch** kwa www.fda.gov/medwatch au piga simu 1-800-FDA-1088.

Nawezaje kujua zaidi?

- Muulize mtoa huduma za afya wako
- Tembelea http://www.cdc.gov/COVID19
- Wasiliana na idara ya afya ya umma ya mahali husika au ya jimbo.

Je, Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA) ni nini?

FDA ya Marekani imeifanya remdesivir ipatikane chini ya njia ya upatikanaji wa dharura unaoitwa EUA. EUA inasaidiwa na azimio la Waziri wa Afya na Huduma ya Binadamu (HHS) hali hiyo ipo kuthibitisha matumizi ya dharura ya dawa na bidhaa za kibaiolojia wakati wa janga la COVID-19.

Remdesivir haijapitia aina sawa ya tathmini kama bidhaa iliyothibitishwa au iliyopitishwa na FDA. FDA inaweza kutoa EUA pale vigezo fulani vinapofikiwa, ambavyo vinajumuisha hakuna mbadala wa kutosha, uliothibitishwa. Aidha, uamuzi wa FDA unazingatia utimilifu wa ushahidi wa kisayansi uliopo unaoonesha kwamba ni muhimu kuamini kwamba bidhaa inakidhi vigezo fulani vya usalama, utendaji, na ulamishaji na inaweza kuwa madhubuti katika kutibu wagonjwa wakati wa janga la COVID-19. Vigezo vyote hivi lazima vifikiwe ili kuruhusu bidhaa kutumika kutibu wagonjwa wakati wa janga la COVID-19.

EUA kwa ajili ya remdesivir ni madhubuti kipindi chaazimio la COVID-19 kuthibitisha matumizi ya dharura ya bidhaa hizi, isipokuwa inapotamatishwa au inapobatilishwa (baada ya hapo bidhaa hazitatumika tena).